

Hutoba Kutoka Wakolosai

Na Andrew Connally

Milango Ya Kitabu	Ukarasa
1. Kristo - Fahari Yake	02
2. Mahubiri ya Paulo	04
3. Jibu la Mungu kwa Makosa ya Mtu	05
4. Kristo - Siri ya Mungu Imefunuliwa	08
5. Kristo - Utimilifu wa Mkristo	10
6. Kutafuta Yaliyo Juu	12
7. Kiumbe Kipyta - 1	14
8. Kiumbe Kipyta -2	16
9. "Neno la Kristo Likae Ndani Yenu"	18
10. Kristo - Kiini Cha Uhusiano wa Nyumbani Mwetu	20
11. Kristo - Kiini Cha Uhusiano Wa Shughuli Zote	22
12. "Msiwe na Uchungu Nao"	23
13. Kutoka Chumba Cha Faragha Mpaka Sokoni	25

KRISTO - FAHARI YAKE.

Wakol. 1:12-23

Azimio: Yesu Kristo anayo fahari katika mambo yote, kwa hiyo, ndiye ujumlisho wa kusudi la Mungu kwa mwanadamu.

Shabaha: Kuonyesha fahari ya Kristo kwa kuonyesha uhusiano wake na vitu vyote.

Dibaji: Katika Wakolosai hoja ya Paulo ni fahari, ukamilifu wa Kristo: Mtume hakuitembelea Kolosai, lakini alifurahia sana na kuungana na wanafunzi wake, ambao, kutoka Efeso, walianzisha kazi huko.

GNOSTICISM, filosofia ya siku zile, ilikuwa ikijiingiza katika kanisa mahali pale. Paulo katika kitabu hiki anapigana na kukanusha fundisho hilo la uonga.

Katika kukanusha Gnosticism, ambayo ilifundisha kwamba Kristo hakuwa Mungu, aliumbwaa mdogo kuliko Mwenye Enzi. Paulo alikutana na filosofia zote za mwanadamu. Hili alilifanya kwa kuonyesha ukamilifu, utimilifu, ufabari wa Kristo.

I. Mungu - Shukrani Kwake Kwa Sehemu Yake Katika Ukombozi.

A. "Aliye wastahilisha" - Katika neema ya Mungu tu tumestahili kusawazishwa, kushiriki pamoja na watakatifu katika nuru. Mungu ni nuru, Yoh. 1:8. Kristo ni nuru, Yoh. 8:12; 12:36; watakatifu ni nuru, Wafil. 2:15-16. Mtu anaposhiriki nuru ya Kristo ndipo awezapo kuonyesha num hiyo, na kwa njia hiyo, hurithi pamoja na hao waliomo katika nuru.

B. "Alituokoa" - War. 7:24-25; Hili pia ni la Mungu. Mungu huhesabia haki. War. 8:33; Mungu anazidisba, Mdo. 2:40; Mungu hupatanisha, 2 Wakor. 5:18.

C. "Ukombozi" - Mungu ametununua tena, Mungu ametuhamishia katika Kristo, 2 Wakor. 5:18. Kwa hiyo, vita vyote ni vya Mungu.

II. Kristo - Chombo Cha Mungu - Utukufu Wake Na Fahari Katika Vitu Vyote.

A. Uhusiano wake na Mungu, mfano, Isa. 9:6-7; Waebr. 1:1-3.

B. Uhusiano wake na Ulimwengu.

1. Mwumbaji, Wakol. 1:15; Yoh. 1:1-3; Waebr. 1:2.

2. Mhifadhi, "jumlisha," "shikilia," Waebr. 1:3.

3. Alikuwako tangu awali pamoja na Baba, Yoh. 1:1; 8:58; Wafil. 2:5-8.

C. Uhusiano wake na Kanisa, Kichwa, Wakol. 1:18; Waef. 1:22-23; Math. 23:8-11; 28:18

D. Uhusiano wake na ufunuo. "Ukamilifu," Wakol. 1:19; 2:9; Tabia na matokeo yote ya Baba, neno na roho vimejumlishwa ndani ya Kristo.

E. Uhusiano wake na wenye dhambi- mpatanishi, njia ya upatanishi, Wakol. 1:20-22; Waef. 2:15-18; 2 Wakor. 5:18-24.

III. Ninyi - Wakati Wenu Uliopita, Uliopo, Unaokuja Unavyohusiana Na Kristo.

- A. Wakati uliopita, mlifarikishwa na maadui, Wakol. 1:21, tazama Waef. 2:11, "nia na matendo mabaya" ya mtu kila siku humtenga na Mungu, Waef. 2:1-3; 2 Wakor. 10:3-5.
- B. "Sasa" - mmepatanishwa, Mst. 22. Kipingamizi cha dhambi kimeondolewa. Njia imefunguliwa, Waebr. 9:23-38; Waebr. 10:19-22.
- C. "Awalete" - watakatifu wasio na mawaa, wasio na lawama. Haya ni matakwa ya Mungu, Mst. 22. Hii ni shabaha ya Kristo. Waebr. 10:23-25.
- D. "Ikiwa" Mst. 23. Wokovu wa mambo yake kila siku.
 - 1. "Mkidumu katika imani," Waebr. 3:12-14.
 - 2. "Mkawa imara," 1 Wakor. 15:58.
 - 3. "Mkiwekwa katika msingi," Waef. 3:17.
 - 4. "Msipogezwa na kuliacha tumaini," Waebr. 6:17-20.

Mwisho: Raya ndiyo yalikuwa maneno ya injili kama yalivyohubiriwa na Paulo. Katika viumbe vyote chini ya mbingu (ni ajabu kwamba walilipeleka katika viumbe vyote? Mst. 23). Ndilo neno la injili leo. Mungu yu tayari na anataka kukuhamisha wewe; Kristo katika ufhari Wake, anakuombea kama mwombezi wako; umefanikishwa na u adui uzidivyo kubakia dhamhini. Kwanini sasa usipatanishwe ill akulete kwake mtakatifu, usiye na lawama? Haya ndiyo maneno na mwito wa injili. Kwanini usiyakubali sasa?

MAHUBIRI YA PAULO

Wakol. 1:21-29

Azimio: Mahubiri ya Paulo yalihusiana na mahitaji ya kila mtu katika kila siku, Hi kumleta kila mtu mtimilifu ndani ya Kristo.

Shabaha: Kuonyesha kipimo cha mahubiri ya Paulo ili kumleta kila mtu mtimilifu ndani ya Kristo.

Dibaji: Mungu ameona vema kujulisha siri tukufu ya injili, ambayo ni "Krista ndani yenu, tumaini la utukufu."

Kusudi la mahubiri ya Paulo lilikuwa ya "kumwonya kila mtu, kumfundisha kila mtu ili amlete kila mtu mtimilifu ndani ya Kristo."

Huu ndio moyo hasa wa injili, 1 Wakor. 15:1-4, na kiini cha tumaini takatifu.

I. Paulo Alihubiri Nini?

- A. Paulo alimhubiri Kristo, ufunuo, na hekima ya Mungu, Wakol. 1:27; Mdo. 9:20; 1 Wakor. 2:1-2; Wagal. 6:14; Mdo. 8:5, 12.
- B. Paulo alihubiri, "Kristo ndani yenu," Mst. 27 Math. 5:16; Kristo akitawala maisha, Wagal. 2:20; 5:24.
- C. Paulo alihubiri, "Kristo tumaini la utukufu," Mst. 27. Yoh. 1:29; 1 Pet. 4:12-13; 1 Pet. 5:4; Yak. 1:12; 2 Tim. 4:8.
- D. Haya yote yanafaa "kumleta kila mtu mtimilifu ndani ya Kristo." Mst. 28

II. Tabia Ya Mahubiri Ya Paulo ..

- A. Mahubiri ya Paulo, "alimwonya na kumsihi kila mtu," Mst. 28.
- B. Hakuna mipaka ya geografia, hakuna mipaka ya biashara, hakuna mipaka ya kabilia, mipaka ya utamaduni, mipaka ya elimu, mipaka ya ume au uke, hakuna mipaka ya dini na Mungu aturehemu sisi tunaoweka mipaka!

Mwisho: Mahubiri ya Paulo yalikutana na mahitaji ya wakati wake na yanakutana na mahitaji ya wakati wetu. Tunalotakiwa kufanya ni kuhubiri kama alivyofanya. Ikiwa tutafanya matokeo yake yatakuwa yale yale. Mungu na atusaidie kwani ni kwa lazima, "tutamleta kila mtu mtimilifu katika Kristo."

JIBU LA MUNGU KWA MAKOSA YA MTU

Wakol. 2:1-23

Azimio: Mungu ametoa jibu kwa kila kosa la mwanadamu ndani ya Kristo.

Shabaha: Kuonyesha kuwa Kristo ndiye jibu 1a Mungu kwa makosa ya mwanadamu kuhusu filosofia ya uongo, Uhalali, Mambo yasiyoelezeka, na mafundisho ya uongo.

Dibaji: Ulimwengu umeenea na makosa ya kila aina. Labda hayajawahi kutokea katika historia ya mwanadamu ambapo wengi wamekosa katika mengi. Kwa hiyo, siyo hapo awali katika historia ya mwanadamu ambapo wengi wamehitaji jibu 1a Mungu kwa makasa ya mwanadamu tu.

Miaka elfu mbili iliyopita Mungu kwa uvuvio alitupatia jibu kwa matatizo yetu yote. Kama vile hatuna muda wa kuzungumzia matatizo ya mwanadamu tunaweza kuonyesha jibu la Mungu katika mahitaji ya mwanadamu katika chache na hivyo kumridhisha mwulizaji kwamba Mungu ametoa majibu yote kwa mahitaji ya mwanadamu na kwamba jibu hilo linapatikana ndani ya Kristo.

I. Makosa Ya Mwanadamu Yanaongezeka

A. Hatari ya filosofia ya uongo. Wakol. 2:8-9.

1. Onya: "Angalieni" kuna maana ya kuwa na kutumia ustadi wa kuona kwa njiia ya kuwa waangalifu. "Filosofia," hasa upendo wa maarifa, iko hapa kwa njia yo yote ya wazo la dini ambalo halina Kristo kama kiini cba mamlaka. Mkristo anaweza "kutekwa" kukamatwa na kuchukuliwa kama mateka. Wazo duni kama hili wakati linapoonekana katika majivuno ya mtu ni la uanzisha.ii wa shetani na "si kwa jinsi ya Kristo." Ni katika Yeye hazina zote za hekima na maarifa zimesitirika." Wakol. 2:3.

2. Dawa: Mst. 9:13, Yesu ndiye ukamilifu wa jinsi ya Mungu, kwa hiyo, hakuna kinachoiaidua chenyeh manufaa kwa Mkristo kinachopatikana mahali pengine pote! fn. Yoh. 1:14; Wakol. 1:19. Katika Krista, utambulikano wa uzima wetu Wa kiroho ultimilika unapatikana, Mst. 10 a; Ndani Yake, lazima uwe utambulikano wa mamlaka yote na nguvu, Mst. 10 b; (Hili linamaanisha kuwa kwake ndiye kichwa cha kanisa, Wakol. 1:18; na fahari katika vitu vyote.) Ndani yake tunayo nafasi mpya, tohara ya washindi katika ufufuo wa Krista, Mst. 12-13, na utii wetu unatupatia maisha mapya.

B. Hatari ya Uhalalisho, Wakol. 2:14-16.

1. Onyo: Mambo halali yakuadhimisha yaliondolewa' katika Kristo. Sheria ya Musa ilifutwa, wakati pazia la hekalu lilipopasuka wakati wa kifo cha Kristo, Math. 27:51; Waehr. 9:13-17. Kristo aliitimiza sheria, Math. 5:17 na kwa kifo chake alituweka nuru kutohana na hukumu zake, Wakol. 2:14. Aliifuta hati iliyokuwa kinyume kwetu. Waef. 2:15-16. Isitoshe, aliangamiza nguvu ya shetani aliyowafunga wanadamu kabla ya wakati, Waehr. 2:14-16. Katika Kristo tunao uhuru kamili.

2. Tamati: Kwa hiyo hakuna sehemu ya sheria ya Musa au ingine He inayomtawala mkristo, Wasabato mjialangalie! Mst. 16. Uadhimisho wote wa sheria ulikuwa kivuli - Kristo ndiye kitu hasa, Mst. 17. Uhatalisho hauwezi kumwongezea lolote mkristo, kwani katika Kristo htiimlika, Mst. 10.

C. Hatari ya Elimu, Mambo ya Siri, Wakol. 2:18-19.

1. Muundo wa kosa, Mst. 18.

a. Hii elimu ya mambo ya siri ilichukua muundo wa gnosticism, maarifa ya uongo ya Iiyozusha unyenyekevu wa uongo na kuhiaribada ya malaika. Hili lilimfanya Kristo kuwa na cheo cha juu zaidi ya watu walioumbika. Mst. 18. Lakini lilikwisha kanushwa, Wakol. 1:15-18; 1:20-23; 2:9-10. Paulo sasa kwa mkazo anawahesabu waalimu wa uongo hao, Mst. 10 b.

2. Sababu ya kosa, Mst. 19. Walikana kuwa Kristo ndiye kichwa. Kichwa na ni kichwa peke yake ndicho kinaweza kuongoza mwili, Mst. 19.

D. Hatari Ya Utawa, Wakol. 2:20-23.

1. Kifo cha mwamini humtenga na kosa la utawa, Mst. 20, fn War. 6:3-4; 6:11. Maadhimisho kama haya huwahuusu makundi ya mamilioni po pote duniani. Kinaamini kazi - ijara badala ya imani - neema kama msingi wa wokovu. Hili hupunguza mkazo wa utu na kazi ya Kristo.

2. Kama tu huru kwanini kukubali? Paulo anasema, "msishike, msionje, msiguse" maagizo haya ya wanadamu. Yaacheni! Hayo ni "maagizo na mafundisho ya wanadamu" na kwa hiyo yatapita! Hayana thamani katika mazoezi ya kupinga dhambi. Hekima ya kweli ni Kristo, Wakol. 2:3, fn. 1 Wakor. 1:30.

II. Kristo - Jibu La Mungu Kwa Makosa Ya Mwanadamu:

A. Mapigano na makosa, Wakol. 2:1-2.

1. "Maumivu" - "kushindana" kukali, utisho wa shetani unafahamu mipaka michache sana, 1 Tim. 4:1-5; 1 Yoh. 4:1-4. Ambalo hasa linatakiwa leo kila mahali! Kumpigania Bwana! Waef. 6:10-12.

2. Magombano ni kwamba sisi kama watu wa Mungu wa farajiwe na kweli, Mst. 2; walioungana katika upendo, Mst. 2; kuwa na siri ya Kristo, Mst. 2.

B. Jibu La Mungu, Wakol. 2:2-7.

1. Siri ya Mungu ni Kristo, Mst. 2. Katika Yeye mna ukombozi na upatanisho wa wanadamu. "Hazina zote za hekima na maarifa" zimefunuliwa kwa wanaoamini, Mst. 3, fn. Waef. 1:9; 3:9.

2. Kristo ndiye jibu katika "maneno ya kushawishi" Mst. 4.

3. Msiondolewe katika "utaratibu wenu na uthabiti wa imani yenu katika Kristo," Mst. 5.

4. "Enendeni katika Yeye," Mst. 6.

5. "Wenye shina, wenye kujengwa mmefanywa imara, kama mlivyofundishwa," Mst. 7.

6. "Mkizidi kutoa shukrani," Mst. 7.

Mwisho: Hilo ndilo jibu 1a Mungu kwa hatari za mwanadamu! Uliamini! Ulikubali! Na Kulifuata! Na ustarehe ukiwa na hakika na imani na wokovu wako! Hakuna kitu katika dunia hii kitakacho kugusa, wala filosofia ya uongo, Uhalalisho, Elimu ya mambo ya siri au Utawa. Wala hutapungukiwa na kitu cho chote kwani haviwezi kukuongezea lolote katika maisha yako - kwani ndani ya Kristo umetimilika! Uridhike!

KRISTO - SIRI YA MUNGU IMEFUNULIWA

Wakol. 1:24; 2:5

Azimio: Yesu Kristo ni Siri iliyofunuliwa ya Mungu, ambayo ndiyo tumaini letu la utukufu, hazina yetu ya hekima, maarifa na fahamu.

Shabaha: Kuonyesha siri ya Mungu iliyofunuliwa katika Kristo.

Dibaji: Katika Wakolosai Paulo anataka kumkweza Kristo, hoja ya kitabu kizima ni ukamilifu wa Kristo, katika Waefeso, hoja ni ukamilifu wa kanisa. Kila mmoja akimstahi mwenzie.

Mwandishi amekwisha onyesha ufahari wa Yesu Kirsto; mfano wa Mungu, mwumbaji na mhifadhi wa ulimwengu mzima, kichwa cha kanisa, alikuwako tangu awali pamoja na Mungu, ukamilifu wa Mungu, mkombozi na mpatanishi wa wanadamu. Sasa ananadharia kazi He ya Mungu ndani ya Kristo katika Mataifa kama ufunuo wa siri ya Mungu.

I. Siri imefunuliwa: Kristo Ndani Yenu, Tumaini La Utukufu, 1:26.

- A. Siri - kufuatana na Paulo ni kweli ambayo kwanza ilisitirika lakini sasa imefunuliwa kwao. fn. Wagal. 1:11-12.
- B. Ilisitirika kwa siku na vizazi, pamoja na kuonekana kwa uhafifu kule ikotokea mara kwa mara, haikujulikana hasa mpaka Kristo alipokuja na kuifunua kwa Mitume. Huduma ya Paulo ilikuwa ya kuifunua kwa Mataifa, 1:25; 1 Wakor. 4:1.
- C. Siri hii sasa ilikuwa ikifahamishwa kwa njia ya Mitume na Manabii kwa njia ya Roho Mtakatifu, Paulo akichaguliwa maalum kama mwenye kuifunua kwa Mataifa, Waef. 3:1-9.
- D. Paulo sasa anakazia kuwa sirl ilikuwa ya kuwaleta Mataifa katika ukumbi mmoja na Wayahudi, Waef. 3: 6-11.
- E. Ni "Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu," Wakol. 1:27; Kristo akidumu ndani yenu, Waef. 3:16; Wagal. 2:20.
- F. Sasa ilikuwa ikifahamishwa kwa njia ya injili, kwa utii wa imani, War. 16:26-27.

II. Kristo - Hazina iliyositirika ya Hekima Na Maarifa, 2:1.3.

- A. Hazina - "mahali ambapo vyombo na vitu vya thamani hukusanywa na kuhifadhiwa; kibweta, sanduku au chombo cho chote ambamo vitu vya thamani vinatunzwa." Thayer.
- B. Hekima - Hekima iliyozungumzwa hapa ni ya mpango wa hekima wa Mungu kwa wokovu wa mwanadamu ikipingana na hekima ya ulimwengu, 1 Wakor. 1:18-24.
 - 1. Ni hekima iliyofichwa kwa ulimwengu kwa muda mrefu, sasa imejulishwa, 1 Wakor. 2:1-2; 2:6-10.
 - 2. Ni hekima iliyofunuliwa ndani ya Kristo, sawa sawa na kusudi lake la milele, Waef. 3:10-11.
- C. Maarifa - Maarifa yanayotakiwa kutuongoza katika njia ya uzima. Ndani ya Kristo yote yamefunuliwa yaliyo ya lazima kuyafahamu mwanadamu; hakuna

haja ya filosofia au hekima ya mwanadamu. Maarifa haya yamejazaliza visomo vya maulizo vilivyo muhimu:

1. Mungu ni nani? Jibu la Yesu, Yoh. 1:18; 14:9. Kumjua Kristo ni kumjua Mungu, ndiye ufunuo. wa maarifa hayo, Yoh. 17:3.

D. Imesitirika - isipokuwa kwa hao wanaokana kuona. Hekima hii na maarifa haya hayapatikani juu, lakini lazima yatafutwe, Math. 7:7. Kama mchuuzi na mtafutaji wa lulu, Math. 13:44-46.

III. Kusudi La Ufunuo Na Ufahamu.

A. Imejulishwa -- kwa utii wa imani, War. 16:26.

B. Imetangazwa - kwa kusihu na kufundisha Hi watu waletwe watimilifu ndani ya Kristo, Wakol. 1:28.

C. Ilielewka - ili yo yote asidanganywe na maneno ya kushawishi, Wakol. 2:2, 4. Boma kubwa la kukinga makosa au kudanganywa ni ufahamu wa kweli.

Mwisho: Tunaishi katika kipindi kikuu cha Mungu kwa mwanadamu duniani; katika kipindi ambamo siri ya Mungu imefunuliwa.

Lakini hata ingawa imefunuliwa katika Mitume na Manabii, na watu wa vizazi vyote wamekuwa na kipimo iulani cha kuifahamu, ni wajibu wa kila mmoja kutafuta ili apate, wapende kushiriki katika mali hasa yaliyowekwa akiba, yenye thamani sana kuliko zote, Yesu Kristo.

Injili ya siri imetangazwa, Je! utaitii imani? Jel utajirekebisha kwayo ili uletwe hali umekamilika? Uielewe ili usidanganywe na makosa? Haya ndiyo mapenzi ya Mungu kwako, na kusudi la kuhubiri. Nani ataikubali?

KRISTO - UTIMILIFU WA MKRISTO

Wakol. 2:8-15

Azimio: Kristo ndiye ukamilifu wa Mungu mwenye enzi na ndani ya Kristo, mkristo ametimilika.

Shabaha: Kuonyesha kuwa hakuna linalopurrgua kama Mkristo yumo ndani ya Kristo.

Dibaji: Tangu mwanzo Ukristo umekuwa na maadui wake; na wamekuwa vivyo hivyo tangu hapo. Miongoni mwa Wayahudi mmekuwa na wenyе kufundisha desturi na dini ya Kiyahudi; miongoni mwa Mataifa mmekuwa na wenyе filosofia. Wagalatia na Warumi wanakanusha desturi na dini ya Kiyahudi; Wakolosai na Waefeso wanapambana na filosofia.

Paulo alitangaza ufahari wa Kristo kuwa ndiye utimilifu wa siri ya Mungu na hazina ya hekima na maarifa. Wakol. 1:26; 2:5. Sasa anafikia katika mashambulizi halisi kuhusu kosa 1a Wakolosai kama linavyopingana na Kristo.

- I. Paulo Aishambulia Filosofia Ikiwa Kama Adui Wa Mkristo Na Kupingana Na Kristo
- A. "Angalieni," Mst. 8 -- Mwe macho.
 - B. "Mateka" - kuchukua mateka, kuchukua mtu kama mahabusi na mtumwa -- Thayer.
 - C. "Filosofia" - kujaribu kubuni kwa mawazo ya mwanadamu ufanuzi wa ulimwengu na uzima. Hekima ya kibinadamu, I Wakor. 1:20-21; 2:4; War. 1:20-23.
 - D. "Madanganyo matupu" - tupu, isiyofaa, bure, na majivuno.
 - E. "Mapokeo ya wanadamu" - mkazo ni juu ya "ya wanadamu" kama wanavyopingana na kile kilicho funuliwa na Mungu. Paulo anasisitiza kuwa hekima na filosofia yake imetokana na Mungu, Wagal. 1:11-12. Mengine yote ni bure, Math. 15:7-9.
 - F. "Mafundisho ya awali ya ulimwengu" - yasio na adabu, ya kitoto, mwanzo wa kweli wa dini na desturi za Kiyahudi, Wagal 4:3-4: au misingi hiyo ya njia za ulimwengu kama ya Mataifa.

II. Paulo Anasisitiza Kuwa Utimilifu Wa Mkristo Ni Ndani Ya Kristo Aliyetimilika.

A. Utimilifu wa Kristo, Mst. 9.

- 1. Sio uiunuo wa sehemu tu ila timilifu: sio maskani ya Mungu kwa sehemu tu, ila kujaa kabisa. Nguvu zote, hekima, na maarifa yote ya Mungu. Upendo, rehema, huruma zote za Mungu. Na chuki yote jinsi Mungu anavyoichukia dhambi na uovu, Yoh. 1:1; 1:18; 14:9.
- 2. Yuko juu ya Malaika na viumbe, wala hivi haviwezi kufananishwa Naye, Waebr. 1:1-5; 1:8-10.
- 3. "Kimiwili" - katika mnofu, Yoh. 1:14; Waebr. 10:5-10; Wafil. 2:5-8.

B. Utimilifu wa Mkristo - Mst. 10-15.

Ndani yake tumetimilika, hamna linalopungua.

Utimilifu :

1. Tohara ya Kiroho, Mst. 11; wa Kiyahudi ulikuwa wa kimwili: mkristo, kiroho, Waefe. 2:11; War. 2:28-29; Wafil. 3:3.
2. Ufufuo wa Kiroho, Mst. 12; "kuzikwa na kufufuliwa" fn. War. 6:3-7; Wagal. 3:26-27.
3. Vzima wa kiroho - Mst. 13; "mfu-mhai," Sasa kiumbe kipyä, 2 Wakor 5:16-17; Waef. 2:1-5; War. 8:12-17.
4. Msamaha wa kiroho, Mst. 13; makosa yamesamehewa, fn. Waebr. 8:12; Mdo. 3:19.
5. Uhuru wa kiroho, Mst. 14. Hati zimefutwa, uhalalisho umekufa! Aliiondoa sheria, kwa hiyo hakuna ambacho yaweza kusaidia katika utimilifu wa mkristo, Waef. 2:14; Waebr. 9:15-17; 10:9-10.
6. Ushindi wa kiroho, Mst. 15; akaharibu mamlaka alimshinda Shetani, Kristo alikuja kumfunga mtu mwenye nguvu, Math. 12:29; aliziangamiza kazi za Shetani, 1 Yoh. 3:8; alizifanya nguvu za Shetani zisiwepo, Waebr. 2:14-15; ambalo Kristo amelifanya sasa, Ufu. 1:18.

III. Kwa Hiyo Mkristo Asihukumiwe –

- A. Katika mambo ya Filosofia, 2:8.
- B. Katika mambo ya dini ya Kiyahudi.
- C. Katika maono ya Malaika na ibada ya mizimu, 2:18-19.
- D. Katika mambo ya Utawa, 2:20:23.
- E. Bali yeche atafute yaliyo juu, Wakol. 3:1-4.

Mwisho: Kitu gani chawenza kuongczwa kwa Mkristo ndani ya Krista (Rudia muhtasari wa kisomo). Maarifa, hekima na uzima wake umetimilika ndani ya Kristo. Adui zake wameanguka, ni mshindi na mkamilifu. Kwanini na wewe usiwe hivyo?

KUTAFUTA YALIYO JUU

Wakol. 3:1-4

Azimio: Katika kuwa Mkristo kuna mabadiliko yaliyo kamili, kutafuta yaliyo juu.

Shabaha: Kuonyesha njia hasa ya uongofu mtu anapoitii injili ya Kristo.

Dibaji: Kuwa mkristo kunahusu mabadiliko yaliyo kamili katika maisha ya mtu. Huwa ili kiumbe kipyta, 2 Wakor. 5:17. Ni mabadiliko kamili "kumrejea Bwana," 1 Wathes. 1:7-9. Kunahusika na kuacha mambo ya thamani na kutafuta mambo yaliyo juu. Uhamisho wa tamaa zetu za dunia hadi katika ulimwengu wa roho.

I. "Basi Mkiwa Mmefufuliwa Pamoja Na Kristo," Mst. 1.

- A. Mtu hufufuliwa pamoja na Kristo ikiwa amezikwa pamoja Naye katika ubatizo, Wakol. 2:12-13.
- B. Katika kuitii injili, mtu huufia uzima wa kale, hufa kwa dhambi, huwa hai kwa haki, War. 6: 1-8.
- C. Kuna usulibisho wa mwili na tamaa zake, Wagal. 2:20; 5:24; 6:14.
- D. Mungu sasa anamtazamia mkristo kuishi kwa roho na sio baada ya mwili, War. 8:12-17.

II. "Yatafuteni Yaliyo luu. Yafikirini Yaliyo luu." Mst. 1·2.

- A. Tafuta tabia mpya.
 - 1. "Vifisheni" - Mst. 5-11.
 - 2. "Jivikeni" - Mst. 12:15.
- B. Tafuteni nia mpya, Wakol. 1:1-2.
 - 1. Mwe na nia ya Kristo, Wafil. 2:5-8.
 - 2. Unyenyekevu, Yak. 4:6-10 1 Pet. 5:5-9.
 - 3. Kujikana, Math. 16:24; Lk. 14:25-27.
 - 4. Utii, Waebr. 5:8-9; Wafil. 2:9.
- C. Tafuteni Ufalme mpya, Math. 6:33.
 - 1. Ufalme wa kiroho, Yoh. 18:36.
 - 2. Maendeleo ya kiroho, 2 Pet. 3:18.
 - 3. Uangalifu wa kiroho, Waebr. 5:12-14.
- D. Tafuteni kazi mpya, Tit. 2:11-14.
 - 1. Kuwarejeza wanaopotea, Wagal. 6:1-2; Yak. 5:19-20.
 - 2. Kufika sehemu za mbali, Math. 28:19.
 - 3. Kuvuna bahati, Wagal. 6:9-10.

III. "Kristo Atakapofunuliwa, Ndipo Na Ninyi Mtafunuliwa Pamoja Naye Katika Utukufu. Mst. 4.

- A. Shukrani kwa Mungu "Atafunuliwa," 1 Wathes. 4:17-18; 1 Yoh. 3:2; Ufu. 1:7.
- B. Mambo ya dunia yatapita, 1 Wakor. 7:31; 1 Yoh. 2:15-17; 2 Wakor. 4: 18.
- C. Mauti na hukumu ni vya hakika, Waebr. 9:27; Mdo. 17:4.
- D. Anakuja pamoja na thawabu Yake, 2 Wathes. 1:3-10; War. 2:2-11; Math. 13:43.

Mwisho: Umepoteza juhudini na muda gani katika kutafuta mambo hayo ya mbinguni? Swali safi ni hili, ni muda na juhudini gani unayoipoteza katika kuchimbua ukweli huu sasa? Umendelea kiasi gani? Unataka kuendelea umbali gani?

Mungu alisema, "Tafuteni!" Na usisahau kamwe!!

KIUMBE KIPYA - 1 (Hotuba Ya Kwanza)

Wakol. 3:1-11; 2 Wakor. 5:17

Azimio: Katika kutafuta yaliyo juu, mkristo huwa Kiumbe kipyta.

Shababa: Kuonyesha tabia za kiumbe kipyta ndani ya Kristo.

Dibaji: Usihi wa "kutafuta yaliyo juu na kuyafikiri yaliyo juu" ni kwa sababu tu viumbe vipyta ndani ya Kristo.

I. Kiumbe Kipyta Ndani Ya Kristo.

- A. "Mlifufuliwa" katika kaburi la maji la ubatizo kuenenda katika upya wa uzima, Wakol. 2:11-12; War. 6:3-4.
- B. Sasa "yatrafuteni yaliyo juu," Math. 6:19-20; 6:33.
- C. "Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu," Mk. 16:19; Waef. 1:19-20.
- D. "Kristo ndiye uhai wetu," Wagal. 2:20; Yoh. 11:25-26.
- E. "Atafunuliwa," I Wathes. 4:16-18.

II. Kwa Hiyo, Mambo Yote Ya Kale Yamepita - Basi Vifisheni:

- A. "Uasherati" -- uhusiano wote haramu, kuuza mwili kwa mwingine kwa ajili ya tamaa, fn. Waef. 5:5-6; Math. 5:31-32; 19:9; Waef. 5:6.
- B. "Uchafu" - maisha yenye tamaa, yasiyo safi, yasiye na adabu, mwenye uchafu, kinyaa, mawazo, maneno na matendo, fn. Math. 5:8; Yak. 4:8; Waef. 5:5.
- C. "Tamaa mbaya" - tamaa za upotovu, mahitaji maovu. Isiyo ya kawaida, au yasio na sheria, fn. Waebr. 13:4; I Wakor. 10:31.
- D. "Mawazo mabaya," mawazo yasiyo na sheria, fn. Math. 5:28.
- E. "Kutamani" - mwenye shauku, mawazo ya uchoyo kupata zaidi kinyume cha sheria au kupata kilichokatazwa, fn. Lk. 12:15; Waebr. 13:5; Wafil. 4:11-13.
- F. "Kutamani ni ibada ya sanamu," ibada kwa mungu wa uongo, Yesu anatuonya, Math. 6:24.
- G. "Hasira" kutofurahia kuliko kukali au motomoto hasa ukiwa na haja ya kuumiza au kuadhibu, fn. Waef. 4:26. Rali ya kuhangashwa.
- H. "Ghadhabu," hasira inayochemka mara moja, si sawa na kurekabishwa kwa hasira, fn. Waef. 4:26.
- I. "Uovu" - chuki ya moyoni, haja ya kuumiza au kuadhibu, fn. Math. 4:43-45.
- J. "Matukano," uchongezi, maneno ya kuumiza jina zuri la mwingine, hata Mikaeli Malaika mkuu hakumchongea Shetani, Yuda 9.
- K. "Matusi," maneno machafu, maneno ya chini chini ya kinyaa, fn. Waef. 4:29; Math. 12:36-37, hujumlisha laana na maneno yasiyofaa.
- L. "Msiambiante uongo," hakuna uongo unaokubaliwa wala kwa Mungu au kwa mwanadamu, wala katika biashara, shule au majumbani, fn. Waef. 4:25.
- M. Utu wa kale umevuliwa. fn. War. 6:12-13.
- N. Utu upya unafanywa upya katika maarifa, 2 Wakor. 4:16; Waef. 4:23-24.

O. Ndani ya Kristo hamna ubaguzi na matengano, Wakol. 3:11; Wagal. 3:27-28.

III. "Kwa Ajili Ya Mambo Hayo Huja Ghadhabu Ya Mungu Juu Ya Wana Wa Uasi."

A. "Ghadhabu ya Mungu itakuja, Waef. 5:6.

B. "Juu ya wana wa uasi," Waef. 5:6.

C. "Katika hayo ninyi nanyi mlitembea zamani," Waef. 5:712; Waef. 2:1-4.

Mwisho: Mkristo anayo kazi kubwa hapo mbele yake kufuta uovu aliouachia kushinda maisha yake. Bila Kristo haitawezekana. Pamoja na Kristo inawezekana na ni lazima kufaulu. Katika au somo linalofuata tutanadharia ambacho lazima kiumbe kipyta "kivae kama kiteule cha Mungu."

KIUMBE KIPYA - 2

(Hotuba Ya Pili)

Wakol. 3:12-17; 2 Wakor. 5:17

Azimio: Kiumbe kipyä katika Kristo 1azima kiongoze usafi au hulka fulani ili kibakie kiaminifu katika Bwana.

Shabaha: Kuonyesha hu1ka ambazo 1azima "tuzivae" katika Kristo.

Dibaji: Misingi ya kutafuta nia mpya na tabia" kwamba mtu yu ndani ya Kristo zinapatikana katika Mst. 3: 1-4. Pia kuna 'kuuvua" kabisa utu wa kale, Mst. 3:5-11. Sasa katika somo hili tunakuja katika 'Kuva'a" kama mkristo, Wakol. 3:12-17.

I. "Basi Kwa Kuwa Mmikuwa Wateule Wa Mungu Jivikenii"

- A. Tu "wateule wa Mungu" Mst. 12. fn. Waef. 1:4-5; Mungu "amewateua" wote watakaoamini na kutii; Yoh. 3:16; 1 Tim. 2:3-4; Mk. 16:15-16. Hawa ndio "waliochaguliwa," wa Biblia. Njia iko wazi kwa kila moja, Mungu anataka wote waoko1ewe, 2 Pet. 3:9. Kila mmoja anaweza kuja atakaye kumtii Mungu.
- B. "Moyo wa rehema," huzuni, huruma, upole, rehema, fn. Math. 5:7. Rehema ionyeshwe katika kuwatumikia wenye kuhitaji, 1 Yoh. 3:17; hili ni muhimu kwani ndiyo itakuwa kipimo cha Hukumu, Math. 25:31-46; Hii ndio dini ya Mungu, Yak. 1:27.
- C. "Utu wema," upole, wororo, utulivu, wema. Utu wema unaweza kila siku kuonekana katika mtu, fn. Wema wa Mungu kwetu. Tit. 3:4.
- D. "Unyenyekevu" - kujiwazia katika unyenyekevu, fn. Wafil. 2:3. Hakuna la kujivunia katika nafsi zetu, Hakuna nafasi ya kiburi na majivuno. Lazima tuwe wapole, Lk. 14:11; Mdo. 20:19.
- E. "Upole" - utulivu wa mawazo unaotaka kumtii Mungu katika hali zote, fn. Musa, Hesa. 12:3 pia Math. 5:5. "Upole" hutafuta matakwa ya Mungu sio ya binafsi. Kristo alikuwa mpole kwa sababu alitaiuta mapenzi ya Mungu, hata hivyo alikuwa na nguvu zote za Mungu na ushujaa, Wafil. 2:5-8.
- F. "Uvumilivu" - kuwa watulivu wakati wa majoribu, udhalimu na mateso. Kuwa wanyenyekemu katika uchokozi. 1 Pet. 2:21-23; Math. 5:38-48; War. 12:19.
- G. "Kuchukuliana" - kuwa na utulivu katika vikwazo na maumivu ya wengine kwa mtu, Waef. 4:2; Waef. 4:2; 1 Wakor. 1:34.
- H. "Kusameheana - TafadhaJi soma Math. 18:21-35. Ikiwa wakristo watajizoeza "Uvumilivu, kuchukuliana na kusameheana karibu kila shida ya kanisa itapotea! Jaribu na uone!"
- I. "Zaidi ya Hayo Yote Jivikenii Upendo," "ndio kifungo cha ukamilifu," kifungo kinachofunga rehema zote pamoja ni "upendo," 1 Wakor. 13: 1-7; War. 13:8-10.
- J. "Amani" - utulivu wa nia na roho. Hakuna vita kati ya Mungu na mwanadamu! Mwisho wa adui, Wafil. 4:7. Amani yaweza kupatikana ndani ya Kristo tu, sio ulimwenguni. "Umoja wa mwili" hufaulu amani hii, Waef. 2:13-18.
- K. "Neno la Kristo Likae Kwa Wingi Ndani Yenu" inawezekana kwa kujifunza tu na maombi, Zab. 119: 11; Zab. 119:148. Soma pia Yer. 23:24; Waebr. 4:12.

L. "Fanyeni Yote Katika lina La Bwana," - kwa mamlaka yake, kwa Yeye na Yeye peke yake anayo "mamlaka yote," Math. 28: 18. Ni kwa njia ya "ndivyo asemavyo Bwana" watu huwa na mamlaka katika dini au maisha. Neno lake ndio msingi wa Hukumu, Yoh. 12:48. Haya ni mamlaka ya Kristo, Neno Lake!

Mwisho: Kiumbe kipyta ni kitu kizuri maehoni pa Mungu na mwanadamu. Huwa kimeumbika katika "mfano" wa Mungu, kinakuwa na tabia za Kristo. Unataka kuwa kama mtu huyo? Unaweza, kwa msaada wa Mungu, Kristo na Roho Mtakatifu nawe pia waweza kuwa kiumbe kipyta.

"NENO LA KRISTO LIKAE NDANI YENU"

Wakol. 3:16-17

Azimio: Neno la Kristo liweze kukaa kwa wingi katika mtoto wa Mungu ili amalize kusudi lake.

Shabaha: Kututhibitishia sisi ili tupiganie kuliwezesha neno la Kristo kukaa kwa wingi ndani yetu na kuonyesha na ambacho litatimiza katika maisha yetu.

Dibaji: Katika historia ya mwanadamu neno la Mungu limekuwa maarufu. Limemjia mwanadamu katika muda wake wa saa za giza na katika nyakati zake za hatari mno. Kila siku neno limejawa na maswali kwa mambo ya kutatanisha kwa mwanadamu. Hata leo ni vivyo hivyo. Neno limekuja. Lipo hapa, linapatikana. Mkristo huhifadhi uhusiano halisi kwa neno la Mungu kwani Mungu amesema, "Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu," na tunadharie neno hili ilivyo na kudumu kwake

I. "Neno la Kristo" - kiwiliwili kizima cha kweli kama ajivyafundisha Kristo, Yoh. 17:17, "Nena la kwe1i, injili," Waef. 1:13. "Neno la kweli la injili," Wakol. 1:5. Neno ambalo ni neno la Mungu, Waebr. 1:1-2; 2:3; Yoh. 14:24.

A. "Likae" - kukaa kunako dumu kwa nia, kuwa na maskani halisi; ya daima. 1 Yoh. 2:14; kama Mungu akaavyo ndani yetu, 2 Wakor. 6:16; kama Roho Mtakatifu akaavyo ndani yetu, War. 8:11; 2 Tim. 1:14, ndivyo neno lazima likae ndani yetu ili tuzae imani "idumuyo" 2 Tim. 1:5. Kwani imani huia kwa kusikia neno, War. 10:17.

B. "Kwa wingi," sio kwa uchache, lakini likae kwa ukamilifu wake, likiwa la nguvu za kuhimiza, kuonya na kuongoza katika maisha yako. Hiti humaanisha upole katika kulipokea. Yak. 1:21. Kulitumia halali, 2 Tim. 2:15; kulijaribu, 1 Wathes. 5:21. Kuwa nalo kwa wingi ni kwa lazima!

C. "Ndani ya mioyo yenu," sio katika nia au akili tu, sio katika kumbukumbu tu, bali katika matakwa na mapenzi yake, "moyo," Zab. 119:11; kama Daudi alivyorudia neno la Mungu: alilitumainia, Zab. 119:42; kwa njia yake alipata fahamu, 119:104; Liliongoza mapito yake, 119:105; Lilimpa mwanga, 119:130.

II. Shabaha Ya Neno Linalodumu.

A. Kukamilisha maisha, kukua kuwa kama Kristo na kwa ajili ya wokovu, 1 Pet. 2:2. Hili liwe lengo la kwanza la Mkristo. Ndicho chakula kinacho mwezesha kukua, Math. 4:4; Yoh. 6:63, 68. Lazima kila mmoja binafsi ashiriki, "kwa ajili yangu." Kwa kukua ndani Yake na neno Lake maombi yetu husikika na kujibiwa, Yoh. 15:7 kwa hiyo, tutaichukua kila njia ya uongo, Zab. 119:104.

B. Kukabili majaribu ya maisha, Math. 4:4,7,10. Kwa neno mtu humpinga ibilisi, Yak. 4:7. Kwalo mtu hujengwa, Mdo. 20:32. Daudi alijiifahamu jambo hili katika siku yake, Zab. 119:11.

C. Kuwafundisha wengine. Kila mkristo lazima a.iitahidi sana kufundisha wengine, kwa sababu ya kushindwa kwa namna hiyo Wakristo wa Kiebrania walikemewa vikali, Waebr. 5:11-14. Huwezi kufundisha usilolijua. Wokovu wa wengine hutegemea juu ya kufundisha, 2 Tim. 3:16-17. Mara nyingi wazazi

wamedharau mafunzo ya nyumbani ya watoto wao, Kum. 6:6-7; Waef. 6:4; Mith. 22:6. Hili litiliwe mkazo na lisiwekewe kisogo.

D. Utumiaji bora wa upanga kukabili maadui wa Mungu. Waebr. 4:12; Waef. 6:17. Kutumia "Silaha za Mungu" mtu lazima azizoe. Daudi hakuweza kutumia silana za Sauli "hakuzikubali" 1 Sam. 17:38-39.

III. Tokeo Halisi Ni Kwamba Mungu Anatukuzwa.

- A. Katika mambo yote utukufu wa Mungu utafutwe, 1 Wakor. 10:31; 1 Pet. 4:11.
- B. Sehemu ya pili hutimizwa katika kuimba, Mst. 16. Sehemu hutimizwa na ibada iyi hiyi kwa Mungu, katika Roho na kweli, Yoh. 4:24. Mungu kutukuzwa kwa maisha ya kiungu wanaowatumikia wengine, Math. 5:13-16. Mungu hutukuzwa kwa jinsi tunavyo ambatana na kweli.
- C. Vitu vyote, basi, lazima vifanyike kwa mama laka Yake, kwa jina Lake, Mst. 17; kwa neno Lake. Lilituzaa, Yak. 1:18; Linaiwezesha ibada yetu, Yoh. 17:17. Linakuwa ndio msingi wa hukumu ijayo, Yoh. 12:48. Kwa hiyo, yote yafanyike kwa jina Lake, yaani mamlaka Yake.

Mwisho: Tukilikubali neno kukaa kwa wingi katika mioyo yetu, tukitawaliwa na kuongozwa na neno Lake, tusijali maisha yetu yataleta utukufu kwa jina Lake. Kama vile hakika maua yanukiavyo vizuri, kama hakika vile juu liwakavyo, ndivyo hata yule anayeenenda katika Neno la Mungu atakavyo mtukuza Baba!

KRISTO – KIINI CHA UHUSIANO

wa

NYUMBANI MWETU

Wakol. 3:18-21

Azimio: Mungu ameteua nyumba ya Mkristo kuwa furaha ya mwanadamu, kwa hiyo uhusiano wetu wa nyumbani uwe na msingi ndani ya Kristo.

Shabaha: Kuonyesha jinsi nyumba ya mkristo itakavyofanya kazi kwa maongozo matakatifu ya Kristo.

Dibaji: Mungu ameteua kitakatifu na kuitakasa ndoa. Mungu aliumba nyumba ya kwanza peponi, na wanadamu wamezifanya kuzimu tangu hapo! Hili ni kwa sababu wanaume, wanawake na watoto wanakataa kuangozwa na neno la Mungu. Nyumba kama anavyoitaka Mungu kuwa ni sehemu ndogo ya peponi. Katika somo hili tunaazimia kurudia kwenye nyumba ambavyo Mungu anaitaka kuwa

I. "Ninyi Wake, Watiini Waume Zenu."

- A. Mungu alimwumba mwanamke kumstahi mwanamume. Mwanamume hakamiliki pasipo mwanamke, Mwa. 2:18-23.
- B. Kuna umoja wa raha na miili vile vile, Mwa. 2:24. Mungu alitazamia umoja wa nia, kusudi na matakwa na upendo.
- C. Ni Mungu anaye waunganisha pamoja, Math. 19:6; ni Shetani ndiye anaye watenganisha, Math. 5:32; 19:9.
- D. Ndoa ishikiliwe kwa heshima na watu wote, Waebr. 13:4.
- E. Useja nj dalili ya ukorofi, 1 Tim. 4:1-3; hata hivyo mtu anaweza kwa utashi wake kuwa towashi kwa ajili ya Ufalme, Math. 19:10.
- F. Wanawake wamearnriwa na Mungu kuwatii waume zao, Wakol. 3:18; 1 Wakor. 11:8-13. Kwa hiyo, mwanamke lazima awe mwangalifu asinyang'anye mamlaka ya mwanaume, 1 Tim. 2:11; 1 Wakor. 14:34.
- G. Mwanamke atawale mambo ya nyumbani, 1 Tim. 5:14, akiwa na nia njema na maisha, 1 Pet. 3:1-6. Na hili likifanyika litakuwa "lakupendeza katika Bwana."

II. "Ninyi Waume Wapendeni Wake Zenu Msiwe Na Uchungu Nao.

- A. Mwanaume ndiye kichwa cha mwanamke, Waef. 5:22-31.
- B. Mwanamke aliumba kwa ajili ya mwanamume, 1 Wakor. 11:8-13.
- C. Mwanamumu lazima aiongoze nyumba yake kwa sheria tukufu, sheria ya upendo, 1 Pet. 3:7. Lazima amheshimu na kumhifadhi mke wake.
- D. Baba lazima aifundishe jamii yake kuheshimu mamlaka, Mith. 3:12; 19:18; 23:13; Waebr. 12:9.
- E. Baba lazima ampende mke wake na watoto, Zab. 103:13.
- F. Lazima aisomeshe jamii yake. Waef. 6:4; Mith. 22:16.
- G. Lazima aihifadhi jamii yake kimwili na kiroho pia. 1 Tim. 5:8.
- H. Kamwe asidharau nyumba na jamii yake, kwani siku moja itakuwa umekawia mno, 1 Wafalme 20:35-43. Lazima tushikilie jamii zetu, 1 Sam. 3:10-14.

III. Ninyi Watoto, Watiini Wazazi Wenu Katika Mambo Yote.

- A. Mungu kila wakati ametaka utii wa watoto kwa wazazi, Kuto. 20: 12. Nyakati huenda zimebadilika lakini sio watu. Huenda labda wazazi watapata heshima kutoka kwa mtoto au wazazi watamtii mtoto. Moja nt njia ya Mungu na ingine ni ya Shetani!
- B. Mungu kila wakati amelaani watoto waasi, Kum. 21:18-21. Hili laonyesha tabia ya Mungu katika kutatii.
- C. Kristo hataki zaidi katika watoto leo, Math. 15:4-6. Huufanya wokovu kutegemea juu ya jinsi tuoavyo watunza wazazi, Mk. 10:19.
- D. Maonyo ya Paulo kwa watoto, Waef. 6:1-3; Wakol. 3:20, mambo yole, siku zote! Unajifungia mlango wa mbinguni mbele zako unapoasi na kutotii!
- E. Fikiria kundi ambamo Mungu atakuweka, 2 Tim. 3:1-2.
- F. Upendo walia nao wazazi kwako lazima ubadilishwe na hata kuondoshwa kama upendo wao siyo sawa na maandiko. Mungu atakubariki kwa wiogi kwa utii na upendo wa ina hii.

Mwisho: Hii ndiyo oyumba jinsi Mungu anavyoitaka. Kila mtu akitimiza wajibu wake katika kuifanya amani, shangwe na furaha. Kushindwa kwa vyo vyote kutaumiza nyumba. Inabarikiwa kwa wingi na kwa wingi mno, kama Mungu anavyotaka.

Kristo – KIINI CHA UHUSIANO
wa
SHUGHULI ZOTE

Wakol. 3:23-4:2

Azimio: Ukristo lazima urekabishe uhusiano wote wa maisha yetu, pamoja na shughuli.

Shabaha: Kuonyesha uhusiano unaotakiwa na Kristo kati ya waajiriwa na waajiri.

Dibaji: Hasa sisi sote lazima tufanye maisha yetu katika njia fulani. Tumegawanyika kama waajiri au waajiriwa. Wote wanao wajibu mbele za Mungu. Bila shaka kama amri zingine zote za Mungu watu watakataa kutawaliwa na kuongozwa nazo, lakini mkristo kila wakati atafute mapenzi ya Bwana wake katika jambo hili na kama katika mengine yote.

I. Jawabu Kamili La Mungu Kwa Huzuni Za Wenye Madaraka.

- A. "Watumwa, tiini katika mambo yote," neno hili wakati huo lilimaanisha Mtumwa, ambalo laweza kutujumlisha sisi sote tulioajiriwa na wengine lea. Hakika hili lina maana ya "kipimo kisichopungua" fn. Waef. 6:5-8; 1 Tim. 6:1-2; Roho ya kutumika na utii.
- B. "Si kwa utumwa wa macho kama wajipendekezao kwa wanadamu." Tit. 2:9-10. Roho ya uaminifu.
- C. "Kwa unyofu wa moyo," utii unaonyeshwa hapa, 1 Pet. 2: 18-25. Roho ya ukweli.
- D. "Mkimcha Bwana," tenda kama kwa Bwana Yeye mwenyewe!
- E. "Lifanyeni kwa mayo," -- sio kwa muda kama anayetaka kusimamiwa! Wahubiri wengi wanahitaji somo hili, kwani mara nyingi huharibu kazi chini ya wazee au katika kusanyiko!
- F. "Mtapokea kwa Bwana ujira wa urithi," Hatimaye Mungu atawalipa wote waaminifu, na kuwaadhibu wote wasiotii, na hata waianyakazi wavivu na wasioaminika katika kuwatumikia watu!

II. Jawabu Kamili La Mungu Katika Taabu Za Wafanyakazi.

- A. "Ninyi akina bwana wapeni watumwa wenu yaliyo haki na ya adili," Waef. 6:9. Mpe kila mtu manufaa ambayo ungetaka, Math. 7:12.
- B. "Mkijua ya kuwa ninyi nanyi mna Bwana mbinguni," Yak. 5:1-6.
- C. "Mkiacha kuwaogofya," Waef. 6:9.
- D. Filemoni na Onesimo na Paulo, Fil. Mst. 4-22.
- E. "Wala kwake hakuna upendeleo," pamoja na Mungu, Waef. 6:9.

Mwisho: Ni kiasi gani cha kilio katika maisha yetu. Tunatafuta kudanganyana katika uhusiano huu lakini yote tunajidanganya 8i9i wenyewe. Wengi wetu tutapoteza roho zetu za milele kwa sababu ya kushindwa katika uhusiano wetu wa shughuli.

"MSIWE NA UCHUNGU NAO"
Wakol. 3:19

Azimio: Ndoa kati ya watu wawili wanaokubaliwa huwa imefungwa na Mungu hadi kifo, au dhambi ya zinaa, imewatenganisha. Yo yote anayeo a kinyume cha mipango hii huyaharifu mapenzi ya Mungu.

- Shabaha:
1. Kuonyesha kinacho fanya ndoa.
 2. Kuonyesha msingi wa Biblia wa talaka.
 3. Kujibu maswali ya kawaida kuhusu soma hili.
 4. Kuwahimiza wote kuiheshimu ndoa na kuishikilia pasipo uhalifu.

Dibaji: Paulo anawasihi waume wote "wapenedi wake zenu msiwe na uchungu nao." Mara nyingine wengi watataka kuwapa talaka wake zao (au waume) na kuoa tena kinyume cha sheria ya Mungu na wakapoteal Ndoa ni ya maana sana na hutawaliwa na sheri a ya Mungu. Mamiloni watapotea kwa sababu walizivunja sheri a Zake kuhusu ndoa, talaka na kuoa tena.

Wala si Biblia kwa ujumla au Yesu mwenyewe, anayependekeza jamii kutokana na kuwa kwa mtu mwenye historia au mwenye elimu ya maendeleo, lakini hasa ni kutoka kwa mwalimu wa dini na tabia. Mkazo ni juu ya ambalo Mungu amelisema, sio juu ya ambalo mtu anafanya au anataka. Mungu ndiye mamlaka ya mwisho katika maisha ya mkristo na kanisa la Bwana.

I. Kitu Gani Kinacho Ifanya Ndoa Ya Maandiko?

- A. Ndoa kama ilivyo imeteuliwa na Mungu, Mwa. 1:18; Waebr. 13:4; Waef. 5:22-23.
 1. Maskani ndiyo yalikuwa kitu cha kwanza duniani, Mwa. 1-3.
 2. Maskani yalianzishwa kwa wema wa mwanadamu, 1 Wakor. 7:2.
- B. Milli yao haina haja ya kuoa, waweza kuwa "matowashi kwa ajili ya ufalme wa mbinguni," Mst. 12.
- C. Maswali ambayo huzuka mara kwa mara kuhusu ndoa zisizo halali.
 1. Je! mtu anaweza kujitetea kuwa ni mjinga wa sheri a za Mungu kuhusu ndoa wakati anapoishi katika dhambi na akaolewa? Soma, Mdo. 17:30-31; 2 Wathes. 1:8.
 2. Je! Sheria za Mungu za ndoa zaweza kuwa kwa "wakristo tu?" Soma, War. 3: 19 na Mk. 16:15-16. Injili ya Kristo ni sheria ya ulimwengu mzima kwa watu wote.
 3. Je! Kuoa wanawake wengi kwaweza kutetewa na ujinga? Kama ni kuwa na wake wengi kwanini isiwe dhambi zote?
 4. Je! Watoto wa ndoa isiyo halali waweza kutumika katika kuitakasa ndoa isiyo ya maandiko? Soma, Ezra. 10:1-17. Je! Mume bado anao wajibu wa "kuwapatia" watoto mahitaji? 1 Tim. 5:8.
 5. Je! Ubatizo unabadili ndoa isiyo ya maandiko kuwa ya maandiko? Kama mtu ni rnwizi na amebatizwa kisha akaendelea katika wizi je, bado ni mwizi?

6. Je! Paulo alitoa msingi mwingine kwa kuoa tena katika 1 Wakor. 7:15? Hasha! Kwani katika mstari wa 11 aliserna, akae asiolewe, au apatane na mwenzi wake!

7. Je! Kila mmoja wa ndoa anao wajibu wa mahitaji ya ashiki ya mwenzi wake? Soma, 1 Wakor. 7:2; 7:3; na 7:4; 7:5.

II. Ni Kitu Gani Kinachofanya Misingi Ya Kimaandiko Kuoa Tena?

A. "Kuacha" hakumruhusu mtu kuwa na haki ya kuoa tena.

1. Sababu ya "kuacha" lazima iwe kwa ajili ya zinaa.

2. Wawili wakitengana na mmoja kaangukia katika dhambi huku hakumweki mwingine kuwa huru kuoa tena kwani kutengana kwao hakukuwa kwa sababu ya zinaa! Kwa sababu Mungu aliwaambia wasiweke vikwazo katika njia ya mwenzi wao, 1 Wakor. 7:2-5. Wote wawili wana hatia. Hakuna aliye huru kuoa tena.

B. Sehemu yenye hatia haiwezi kuoa tena. Wabakie katika useja, au wapatane na wenzi wao, 1 Wakor. 7:11; Math. 10:12.

C. Je! Mtu akimwua mkewe anaweza kutubu na kuoa tena? Je! Unaweza kutenda dhambi kwa makusudi tu ili utubu baadae ukawa huru na kujiburudisha katika uovu wako wa kwanza?

D. Vipi na matanguo? Matanguo ni ustadi wa mwanadamu. Kama walioana kimaandiko basi sheria za Mungu za ndoa zinahusika.

Mwisho: Dawa yake nini kwa matatizo yote kuhusu ndoa, talaka na kuoa tena?

Waelekeze watu kwenye neno la Mungu. Wafundishe watu kabla ya ndoa alilosema Mungu. Wafundishe waliokwisha oana kupendana. Wafundishe kuziheshimu ndoa zao na wasihalifu sheria ya Mungu. Wafundishe kwamba Mungu bado angali anachukia "kuachana." Wafundishe afadhali kuteswa kuliko kutenda dhambi. Wape msaada walio na matatizo ya ndoa. Pinga utukuzaji wa dhambi hiyo mbaya katika maisha yetu. Usimpe nafasi ibilisi. Ikimbie zinaa!

**KUTOKA CHUMBA CHA FARAGHA
MPAKA SOKONI**
Wakol. 4:2-6

Azimio: Mkristo lazima apoteze muda mrefu sirini pamoja na Mungu katika maombi, Hi aweze kuenenda na kunena wazi kama Mungu anavyo mtarajia kufanya.

Shabaha: Kuonyesha namna "ombi, kuenenda na kunena kunavyoungana pamoja katika maisha ya Mkristo.

Dibaji: Somo hili la mwisho katika Wakolosai linagusia mUsho miwili ya maisha yetu. Wa kwanza unahusika na maisha yaliyofichwa ya sala, ambayo lazima yamtambulishe mtoto ye yote wa Mungu. Wa pili na tatu kwa nje, maisha ya shughuli sokoni na mtaani. Kwa hiyo Mungu anaileta miisho hii pamojaa katika sura hii. Tuenende hivyo katika njia za vumbi za maisha ill tuwe mahali pa siri pa Mwenye Enzi!

I. Maonyo Kwa Ajili Ya Maisha Yaliyofichwa Ya Sala Daima, Mst. 4:2-4.

- A. "Dumuni sana," ---- kama uvumba uliozungukwa na watenda kazi katika kihema, vivyo harufu ya maombi imzunguke mkristo wakati wole. Waef. 6:18; War. 12:12; Wafil. 4:6; 1 Wathes. 5:16-18; 1 Tim. 2:1; Lk. 18:1, 8. Ombi ni kitu cha siri. Math. 6:5-6.
- B. "Mkikesha katika kuomba," - kuna hatari ya kufanya katika hali ya usingizi lo lote tufanyalo daima, Math. 26:21; Mk. 13:33; tunahitaji kujitia nguvu kuwa tayari na kuishi katika nia safi. Waef. 5:14.
- C. "Na shukrani" - ombi lote liwe na muundo wa shukrani, Wafil. 4:6; 1 Wathes. 5:16-18; Walkol. 3:15.
- D. "Mkituombea na sisi pia." Paulo mara kwa mara aliomba maombi ya watakatifu ili aimalize kazi ya Bwana. 2 Wathes. 3:1.

II. Maonyo Kwa Ajili Ya Mwenendo Wa Wazi Wa Mkristo Sokoni, Mst. 4:5.

- A. "Enendeni" - tabia ya maisha ya mtu, Waef. 4:1; 5:1; 5:15
- B. "Walia nje" - inamaainsha "kuwa ndani" na "nje." Utotauti huo huo unaonekana katika 1 Wakor. 5:12-13. "Walia ndani" lili wale walia zaliwa tena, Yoh. 3:3-5; walio hamishiwa, Wakol. 1:12-13.
- C. Mwenende kwa hekima - hekima kushindana na ujanja (Ustadi), 2 Wakor. 4:2.
 - 1. Maisha yetu ndio Biblia yao. 2 Wakor. 13: 1-3.
 - 2. Kristo alikula na watoza ushuru na wenye dhambi bali kwa kuwaokoa.
 - 3. Paulo alikuwa halj zotc kwa watu wote ili aweze kuwaokoa wengine, 1 Wakor. 9:22. Angalia ni hatari hili!
 - 4. "Mkiukomboa wakati" - kununua nafasi. Kuchukua wasaa kwa ajili ya Mungu! Nadharia uthamani wa wakati. Nafasi ikipotezwa mara moja haiji tena. Mkristo aitumie kila dakika kwa hekima.

III. Maonyo Kuhusu Maneno Ya Neema, 4:6.

- A. "Maneno ya neema" -- ni maneno yanayoleta au kutengeneza kupendana. Lk. 4:22.

- B. Maneno yetu yanatusaliti ikiwa kwa mema au mabaya, Matn. 26:73. Angalia, Math. 12:34-37.
- C. "Yakikolea munyu," - yanayookoa, Waef. 4:29; Waebr. 13:15. Angalia. Waef. 5:4. Maneno ni muhimu!
- D. "Kujibu ipasavyo" - kuwaambia watu wanaloataka kusikia, yatakayo nufaisha roho zao, mara nyingi hawatayapenda, lakini neno la Mungu mara kwa mara hukata, Waebr. 4: 12. Mkristo kila siku lazima awekwe kwa kuitetea injili, Wafil. 1:16; tayari kutoa jibu kwa kila mtu. 1 Pet. 3: 15; tayar, kushinania imani, Yuda 3.

Mwisho: Tunapofikiria muda uliotumika baina ya wale wa dunia. Na hesabu ya matendo tunayo yatenda. Na maneno tunayoyasema, jinsi gani tunafikiria kuhitaji maombi ya daima! Ombi - matendo - maneno. Kuenenda kwetu na kukutana na mwatiko wa sokoni kutokane na vyumba nya faragha nya maombi.